**Learning by Ear - Illiteracy**

**“A Girl Finishing School”**

**Episode 02: ‘’Mfadhili wa  Latifa’’**

**Author:** Frédéric GAKPARA

**Editor:** Yann Durand

**Translator:** Anne Thomas/Omar Babu-Thelma Mwadzaya

**Characters:**

**Latifa** *(Ana umri wa miaka 15 , ni binti ya Papa Wali na Mamoua. Anasoma shule mwaka wa tisa. Ni mwerevu wala hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo inambidi kukabiliana na uamuzi wa wazazi wake wa kumkatizia masomo anapojiandaa  kufanya mtihani wake.)*

**Zakia** *(Ana umri wa miaka 20, ni msichana aliye na uhuru wa kujitendea mambo, ni rafiki yake Latifa na ameajiriwa katika afisi ya wakala wa Utalii kutokana na tajriba yake ya kimasomo. Ni msichana aliyebahatika kutembelea mahali pengi na hukutana na watu wengi kazini mwake.)*

**Elinam** *(Ana umri wa miaka 19, ni mwanao Papa Wali na Mamoua, ni kaka yake Latifa. Hivi karibuni amejiunga na chuokikuu katika jiji kubwa kilomita kiasi 120 kutoka mji mdogo wanakoishi wazazi wake)*

**Papa Wali** *(Baba wa watoto watatu, mwenye umri wa miaka 52 – Mtoto wake wa kwanza wa kiume anaitwa is Elinam, kisha anafuatwa na binti aitwaye Latifa, na mwisho mtoto wa kiume aitwaye Jaurès. Anashughulika na karakana ya vyuma lakini hajui kusoma na kuandika. Biashara inamwendea vibaya kila kukicha kwa kuwa hajamudu kujifunza mbinu mpya za ufundi hivi kwamba hamudu ushindani mpya wa kibiashara.)*

**Mamoua** *(Mwenye umri wa 39, mke na mama ya watoto wa Papa Wali. Ni mjamzito wa mtoto wao wa nne. Hajui kusoma na kuandika. Anafanya biashara ndogo ya kuuza uji wa unga wa mahindi mbele ya nyumba yao.)*

**INTRO:**

Hamjambo na karibuni kwenye Makala ya pili ya Noa Bongo Jenga Maisha yako ya **"Mtoto wa Kike ahitimu**" yanayoangazia masuala ya kutojua kusoma na kuandika pamoja na elimu. Latifa ni binti yao Papa Wali na Mamoua. Msichana huyo mwenye umri wa miaka 15 yuko katika mwaka wake wa tisa wa shule,ni mwerevu na wala hajawahi kurudia darasa lolote. Hata hivyo inambidi kukabiliana na uamuzi wa wazazi wake wa kumkatizia masomo kwani wameshindwa kumlipia karo.Tangu mamake alipomwambia habari hizo, Latifa anahangaika juu chini kupata mtetezi kwa wazazi wake. Sasa amelazimika kuutafuta ushauri wa rafikiye wa chanda na pete, Zakia. Zakia ni mcheshi aliye na umri wa miaka ishirini hivi anayefanya kazi katika kampuni kubwa ya utalii.Tuisikilize makala ya pili: Nani atakayegharamia elimu ya Latifa?

**<u>Scene 1, IN ZAKIA'S ROOM</u>**

Zakia na Latifa

1. **SFX ATMO: BACKGROUND SOUND OF MUSIC CHANNEL ON TV**

2. **Zakia:** **(Indignantly)** Eti umesema nini, Latifa?

3. **Latifa:** **(Very downtrodden, after a moment's silence)** Kwamba ninataka kuendelea na masomo yangu. Mimi sitaki kuwa kama yeye, Zakia!

4. **Zakia:** Kweli! Huo ndio mtazamo mzuri! Mambo yataka hivyo! Hata sikifahamu anachokifikiria Mamako.Msichana yupi wa kisasa asiyetaka kufanya kazi katika shirika kubwa,awe huru na kujikimu maishani?

5. **Latifa:** Mtazamo wa mama ni wa kizamani. Hata huo uji anaouza nje ya nyumba yetu, mimi ndiye niliyemhimiza aianze biashara hiyo!

6. **Zakia:** Ilikuwa rahisi kwako kumshawishi babako kugharamia kila kitu,matumizi yake ya kibinafsi. Mambo ya kizamani.Mambo yaliisha vipi?

7. **Latifa:** Aliniambia nikitaka niuze nguo zangu ndio nijilipie karo. Alipoyasema hayo niliondoka akalalamika kwamba namfanyia ujeuri .

8. **Zakia:** Unasema kweli? Usife moyo Latifa! Na babako asemaje kuhusu jambo hilo?

9. **Latifa:** Utadhani hayupo, Zakia. Hakunitopoa na alipoondoka alijifanya kwamba alikuwa na haraka ya kuondoka.

10. **Zakia:** Unadhani ni uamuzi wake?

11. **Latifa: Hesitatingly**) Sijui… Sidhani… Tangu biashara yake ilipoanza kuzorota amekuwa akimnyenyekea mama ambaye naye siku hizi ndiye mwenye usemi mkubwa hasa ukizingatia kuwa biashara yake ya uji imeimarika .

12. **Zakia:** Mbona usizungumze na kaka yako? Pengine atakuunga mkono. Ebu fikiria, ati wewe uache masomo ili yeye aendelee na masomo. Hiyo si haki hata kidogo! (**A moment of silence**)

**(Latifa whimpers. She can't hold back her tears. There is emotional music on TV.)**

13. **Latifa:** **(Bursts into tears….)** Nifanye nini?

14. **Zakia:** Mbona unalia? Unafanya nini, Latifa? Huu si wakati wa kujitia dhiki, (**In a tender voice**) Nitazame.Kila mtu hukabiliwa na wakati mgumu maishani.Ndiyo ya ulimwengu.Muhimu zaidi ni kutokata tamaa.

15. **Latifa:**(**Whimpering**) Mimi nimekuwa nikijitahidi sana nisiwaudhi wazazi wangu. Mimi hufanya juu chini nisiwasababishie gharama zisizofaa, Zakia (**tears**).

16. **Zakia:** Nakuelewa. Umevunjika moyo,mpweke na unahisi kwamba umekosewa.... Ninaweza kukusaidia kulipa karo yako. Lakini wazazi wako wasipokubali, itakuwa vigumu....

17. **Latifa:** (**Calmer**) Nashukuru kwa msaada wako. Ni sawa kwako kuchukua tahadhari.Mamangu hawajahi kukuchangamkia, na hivyo wewe ukinisaidia huenda hali ikawa mbaya zaidi.

18. **Zakia:** Mama yako! (**Imitating Latifa's mother**) “Mungu asinijaliye nimpe jina la Zakia binti yangu. Msichana wa watu hana adabu! ZAKIA!(**Swearing**) Tsss!!! Hukuona wasichana wengine wa kufanya urafiki nao ila huyo. Mtizame anavyovaa. Kila unapomwona utafikiri anatembea uchi. Je anajua hata kupika?” (**Bursts into laughter**)

19. **Latifa:** (**Laughing**) Unazungumza kama yeye! (**Laughing again, then silence**)

20. **Zakia:** Tusikae hapa kutwa nzima kujihangaisha. Tumpigie simu kaka yako. Nipe nambari yake ya simu!

21. **Latifa:** Nadhani imo kwenye kitabu changu cha nambari za simu...

22. **SFX ATMO: Opens her bag and looks for her diary, leafs through it.**

23. **Latifa:** Ndiyo hii…

24. **Zakia:** Mambo mazuri! Tafadhali izime runinga.

25. **SFX ATMO: TV is turned off**

**<u>Scene 2, IN ZAKIA'S ROOM</u>**

Zakia, Latifa and Elinam **(on the telephone)**

26. **SFX ATMO:** **sound of mobile phone keypad and ringing.**

27. **Zakia:** Inalia! Shika simu. Zungumza naye. Mweleze kila kitu taratibu.

28. **Elinam:** Hallo!

29. **Latifa:** Hallo Elinam, Mimi hapa Latifa.

30. **Elinam:** Vipi Latifa, mambo?

31. **Latifa:** Poa.

32. **Zakia:** (**Whispering to Latifa**) Utasemaje uko poa? Mwambie kwamba mambo si mazuri kabisa.

33. **Elinam:** Uko wapi?

34. **Latifa:** Nyumbani kwa rafiki yangu Zakia. Ninatumia simu yake ya mkono.

35. **Elinam:** Watu wote hawajambo?

36. **Latifa:** Hawana neno. Naam, lakini nilifukuzwa shule jana kwa kuwa karo haijalipwa. Naye mama asema niache masomo.

37. **Elinam:** Wasemaje? Kwa nini?

38. **Latifa:** Kwasasabu yeye na baba hawawezi kunilipia karo.

39. **Elinam:** Unasema nini eti?

40. **Latifa:** Leo asubuhi mama aliniamsha na kuniarifu eti baba anahitaji fedha kukulipia wewe kodi ya nyumba.

41. **Elinam:** Ati nini? Kodi yangu?

42. **Latifa:** Naam.

43. **Elinam:** Wala hilo si tatizo! Hajaniletea fedha zozote kwa muda wa miezi mitatu na bado ninaendelea vyema. Ulimwambia nini mama?

44. **Latifa:** Nimesema siwezi kukatiza masomo yangu kwa hali yoyote ile. Kwa hivyo mama ameniambia niuze nguo zangu ili nijilipie karo.

45. **Elinam:** (**Ironically**) Ajabu, Wazo zuri sana hilo!
(**Laughing**)

46. **Latifa:** Unadhani hivyo?

47. **Elinam:** Hata! Ninakutania!

48. **Latifa:** Mbona usiwapigie simu uwarai wabadilishe msimamo wao?

49. **Elinam:** Nitawapigia simu kesho. Hivi sasa simu yangu haina fedha za kutosha

50. **Latifa:** Subiri. Zakia ataka kuzungumza nawe.

51. **Elinam:** Sawa, mpe simu.

52. **Zakia:** Hujambo Elinam.

53. **Elinam:** Sijambo Zakia, habari gani?

54. **Zakia:**Habari si nzuri. . Latifa hajakoma kulia. Tafadhali msaidie. Nitatafuta fedha za kumlipia karo lakini itakubidi ujifanye kwamba fedha hizo ni zako.

55. **Elinam:** Asante sana kwa msaada wako, Zakia. Wewe ni rafiki wa dhati. Mimi mwenyewe ninatafuta ufadhili. Nikifaulu, mambo kutakuwa na ahueni.

56. **Zakia:** Usijali, utapata ufadhili – Una haki ya kupewa!

57. **Elinam:** Asante! Kesho nitawapigia simu wazazi wangu kisha nitakuarifu itakavyokuwa.

58. **Zakia:** Sawa! Tutangumza hiyo kesho basi!

59. **Elinam:** Haya. Kwaheri, Zakia!

60. **Zakia:** Kwaheri, Elinam! **(Switches off the phone)** Mambo mazuri! Ninaamini mambo yako yatakwendea vizuri, Latifa!

61. **Latifa:** **cautious)** Unadhani hivyo? Ukweli?

62. **Zakia:** Acha hayo nawe, twende tukapunge upepo kisha nitakupeleka nyumbani.

63. **SFX: Noise of chairs being pushed in, the steps of the two girls, the door being locked.**

64. **ATMO: TOWN. TRAFFIC.**

65. **Latifa:** Tunaelekea wapi, Zakia?

66. **Zakia:** Tuingie mjini kidogo.

67. **Latifa:** Lakini ninapaswa kuwa nimesharejea katika kipindi cha saa moja hivi.

68. **Zakia:** Usiwe na wasiwasi, tutawahi.

69. **SFX: MOPED BEING STARTED**

## MUSIC

**<u>Scene 3, AT PAPA WALI'S HOME</u>**

Papa Wali, Mamoua, Latifa and Elinam **(on the telephone)**

70. **ATMO: HENS IN THE YARD, SHEEP IN THE DISTANCE, LITTLE TRAFFIC, SOUNDS OF POTS AND PANS, CHILDREN SHOUTING**

71. **Mamoua:** Uji wa moto! Mama Mamoua huyu hapa nje! Uji moto huu hapa wauzwa.(**Mamoua's shouts go on**)

72. **SFX: MOBILE PHONE RINGS FOR A LONG TIME. FOOTSTEPS AND SOUND OF OBJECTS BEING MOVED**

73. **Papa Wali:** Kwani nimeiacha simu yangu wapi? (**Silence. He calls his daughter**) Latifa!

74. **Latifa:** **(From afar)** Beeeeh!

75. **Papa Wali:** Simu yangu inalia. Iko wapi?

76. **Latifa:** **(From afar)** Uliiacha karibu na karo.

77. **Papa Wali:** Sijui nina nini mimi!

78. **SFX: Fast steps. PHONE RINGS STOPS AS HE ANSWERS**

79. **Papa Wali:** Hallo!

80. **Elinam:** Hallo, Baba! Shikamoo ni mimi, Elinam.

81. **Papa Wali:** Marahaba mwanangu! Hujambo?

82. **Elinam:** Sijambo, Baba! Nyumbani hawajambo?

83. **Papa Wali:** Hawana neno. Nasikitika sijaweza kukuletea fedha zozote hivi karibuni. Mwenye nyumba nadhani ameanza kukutatiza.

84. **Elinam:** Ninajikaza vivyo hivyo, baba. Hata hivyo hiyo siyo sababu yangu mimi kukupigia simu. Ni kuhusu Latifa. Najua amefukuzwa shule.

85. **Papa Wali:** Ndiyo, lakini tumeshatatuwa mambo yake.

86. **Elinam:** Mmetatua vipi?

87. **Papa Wali:** Atakatiza masomo yake ili amsaidie mama yake kwenye biashara yake.

88. **Elinam:** Lakini hapo alipo ana umri wa miaka 15. Anatakikana kufanya mtihani wake mwaka huu!

89. **Papa Wali:** Wajua vizuri kwamba sijaweza kukuletea chochote cha kusimamia kodi yako na gharama zako nyingine. Kwahivyo mahitaji ya Latifa hayako juu kwenye orodha yangu kwa sasa .

90. **Elinam:** Baba usimtatize Latifa kwa sababu ya matatizo yanayotukabili. Ninajitahidi kadri ya uwezo wangu kukaa vizuri hapa katika chuokikuu.

91. **Papa Wali:** Elinam, nataraji hujaanza maisha ya ombaomba ili uweze kusalia katika chuo kikuu. Una maana gani unaposema unajitahidi kukaa vizuri chuoni?

92. **Elinam:** Baba, simwombi mtu. Lakini niko tayari kuwa ombaomba kwa ajili ya mdogo wangu.

93. **Papa Wali:** Mamako ni mjamzito. Hawezi kurauka kupika uji wake. Inambidi Latifa amsaidie kwavile sina fedha za kuajiri mfanyakazi.

94. **Elinam:** Naomba nizungumze na mama tafadhali!

95. **Papa Wali:** Haya! (**He calls his daughter**) Latifa!

96. **Latifa:** Beeh?

97. **Papa Wali:** Mpelekee mama yako simu hii. Ni kakako huyo. Anataka kuzungumza na mamako. (**To Elinam**) Subiri!

98. **SFX ATMO:** **Fast steps of young girl. Sounds of a calm road.**

99. **Latifa:** Mama, Elinam ataka kuzungumza nawe.

100. **Mamoua:** Eh! Eh! Eh! Mwanangu! Bahati iliyoje leo! (**In the phone**)Hallo!

101. **Elinam:** Shkamoo Mama! U hali gani?

102. **Mamoua:** Sijambo ila ninajisikia mchovu. Na wewe je? Natumai huna neno.

103. **Elinam:** Sijambo Mama. Nimepiga simu hii kwasababu ya Latifa. Singependa akatize masomo yake. Baba amenipa sababu nyingi ila sijapata moja ya kuniridhisha. La msingi ni Latifa arejee shuleni!

104. **Manoua:** Elinam, baba yako anakabiliwa na matatizo mengi. Unafahamu kwamba hivi karibuni watazikata nguvu za umeme kwenye karakana yake? Ikiwa hakuna umeme atalazimika kulifunga duka!

105. **Elinam:** Baba asema sababu ni wewe huku wewe wasema yeye ndiye sababu. Lakini ni nani atafaidika endapo Latifa atakatiziwa masomo yake?

106. **Mamoua:** Elinam!

107. **Elinam:** Mama, simu yangu inaisha fedha. Mwambie baba nitamwandikia barua. Hatahivyo mama nimeshakupa mtazamo wangu. Kwaheri mama!

108. **Mamoua:** Elinam? Kwani umekasirika? (**No answer**) Oh, amekata simu tayari (**Alone**) Hapa yalipofikia bora kuyasawazisha, sitaki kuzozana na mwanangu...

**MUSIC**

**OUTRO**

Je, Elinam atapata fedha za kutosha kuweza kuyabadili mawazo ya wazazi wake? Ataweza kumsaidia mdogo wake Latifa aendelee na masomo yake? Barua ya Elinam itafafanua kipi? Majibu utayapata katika kipindi kijacho cha mfululizo wa “**Mtoto wa kike ahitimu**” , makala inayoelzea tatizo la kutojua kusoma na kuandika na Elimu. **Ukipenda kusikiliza vipindi vyote vya mfululizo wa Noa Bongo jenga maisha yako, tazama ukurasa wetu wa tovuti www.dw-world.de/lbe. Unaweza pia kutuandikia barua-pepe kupitia anwani:** lbe@dw-world.de

**Ahsante kwa kutusikiliza. Hadi mara nyingine tutakapokutana tena nakutakia kila la kheri!**

## END OF 2nd EPISODE